# Learning by Ear – Religious Dialogue: "A Bridge over Gori"

## Episode 09: "Maridhiano''

**Author: Romie Singh**

**Editors: Katrin Ogunsade, Naïma Guira**

**Proof reading: Natalie Glanville-Wallis**

**Expert on African religions: Jean-Félix Belinga Belinga**

**KISUAHELI ERIC PONDA/THELMA MWADZAYA**

**List of characters for episode 9:**

- Narrator /Philip, male (17)
- Harry, male (17)
- Layla, female (16)
- Mat, male (17)
- School Director, Mrs Milulu, female (48)
- Father Barnabus (Harry's Uncle), male (49)
- Chief Dembele (Harry's father), male (51)
- Layton-Browne (Philip's father), male (50)
- Hassan, male (12)
- + Students

1. **SIG TUNE UP**

2. **INTRO:**

**Hujambo na karibu kwenye sehemu ya tisa ya mfululizo huu wa vipindi vya Noa Bongo-Jenga Maisha Yako katika mchezo wa ''Daraja la Gori''. Huu ni mchezo unaosimulia hadithi ya kusikitisa jinsi Siasa na Dini zinavyoweza kutumiwa kuzua uhasama baina ya jamii mbili, Familia mbili na wapenzi wawili Harry na Layla ambao wanaolazimika kulificha Penzi lao changa.Ungana na mabingwa wetu wanapoutambua umuhimu wa kujadiliana,ushirikiano na kuvumiliana.Katika makala ya leo ya "*Maridhiano"* Layla ana mpango ulio na azma ya kuutafutia mzozo wa ardhi suluhu.Msikilize Philip:yeye ni mmoja wa marafiki wa dhati wa Harry na ndiye msimulizi wa kisa chote.Baki nasi hadi tamati ufahamu iwapo Layla atafanikiwa!**

**Scene 1. In the Big Hall**

Philip, School Director, Students

3. **UBUNTU COLLEGE ANTHEM (FADE IN AND HOLD UNDER)**

**4. PHILIP/NARRATOR: Niliwasili kwenye mkutano wa asubuhi nikiwa na moyo mzito.Nilimsaliti rafiki yangu mkubwa,kwasababu ya msichana ambaye hata sikumfahamu vyema.Layla ni msichana Mrembo na aliyenivutia kwa haiba yake,urembo wake na akili yake. Baada ya Mkurugenzi wa Chuo kuikariri dua ya asubuhi iliyoandikwa na Mtawa wa KiTibet....nilipata ufahamu mpya.Nilijiona na mapungufu na nilikuwa na mengi ya kujifunza.**

***5.* DIRECTOR: (reading) Maishani, lazima ufahamu, kama lilivyo tone la mvua.Ni kitu kinachopendeza ila uzuri wake hutoweka pale linapokamilika.Kwahiyo yaweke malengo yako,utumie muda wako vizuri,si usiku si mchana.**

**6. <u>SFX: Murmur of students</u>**

**7. DIRECTOR:** **Maneno haya ya busara wakati wa asubuhi, yanatutia moyo tuyafikirie maisha,thamani yake na tunavyoishi kwa jumla.Tumeshuhudia visa vingi vya uhasama ulio na misingi ya kidini katika bara hili. Tumeshuhudia mauaji, na misikiti na makanisa yameteketezwa kwa madai ya kumcha Mungu.Kwa hapa Gori, dhamira yetu ni kuuonyesha umma kuwa kuna njia nyengine:ya majadiliano,kubadilishana mawazo pasina hofu pamoja na uongozi bora.Sasa kuna pendekezo la kuiadhimisha siku ya Mapatano katika kipindi cha miezi mitatu ijayo.Baraza la mji linaandaa tamasha la siku mbili litakalowashirikisha wakazi wake wote pamoja na wanafunzi wa shule.Kutakuwa na mashindano ya Mjadala na michezo kwa ajili ya kusherehekea mchango wa viongozi wa siku zijazo.*(Laughter).Hayabasi n*awatakia siku njema.**

**8. <u>SFX: LAUGHTER AND APPLAUSE FROM STUDENTS</u>**

**<u>Scene 2. In the school garden</u>**

**Harry, Mat, Philip, Layla, School Director**

**9. <u>SFX: Birds, students laughing and talking of students from a distance</u>**

**10. HARRY:** *(sadly)* **Layla hanisemeshi...Mat!**

**11. MAT:** **Kwani umemkasirisha Harry**?

**12. HARRY:** *(sadly)* **Ni jambo dogo tu.Tazama – Bi Milulu ameandamana na Layla— Na wanakuja huku!**!

**13. <u>SFX: Footsteps (2 people) on concrete</u>**

**14. ALL:** **Habari ya Asubuhi Bi Milulu!!**

**15. DIRECTOR:** **Habari Harry…Mat.. Philip…. Layla ana pendekezo la maadhimisho ya siku ya Mapatano...Layla waeleze tafadhali.**

**16. LAYLA:** Naam, … nilikuwa nikiwaza iwapo tunaweza kuziandaa sherehe hizo za siku mbili katika ardhi ile inayotishia kuzitenganisha jamii na familia zetu…Harry?

**17. HARRY:** Kweli Layla hilo ni wazo zuri sana!

**18. MAT:** Kama ishara ya maridhiano? Wazo zuri sana!

**19. DIRECTOR:** Philip? Umenyamaza sana. Una mtazamo gani? Babako ana ushawishi mkubwa sana kama mhariri wa gazeti maarufu la Gori.

**20. HARRY:** Jee anaweza kuunga mkono kampeni kwenye gazeti lake?

**21. PHILIP:** ….Kwa lengo la kulizuwia kundi lolote lile la kidini kuwa mmiliki wa ardhi hiyo?Naamini ataliunga mkono hilo.Nitamuuliza.

**22. DIRECTOR:** Kumbukeni bado hisia za watu zimepamba moto.Jee jamii yetu iko tayari kwa maridhiano?Harry?

**23. HARRY:** **Nimekuwa nikimshawishi Baba mdogo amsamehe Hassan na pia ayafutilie mbali malalamiko aliyo wawasilishia maafisa wa Polisi.**

**24. LAYLA:** *(surprised)* **Harry – Kweli umefanya hilo?** *(happy)* **Ohhh… Harry!**

**25. MAT:** **Hata hivyo lazima mtu aadhibiwe kwa jaribio hilo la kuliteketeza kanisa.**

**26. HARRY:** **Ni kweli ila nilidhani ingekuwa bora zaidi tukizingatia adhabu ya huduma kwa jamii.Hassan-na sisi sote pia-tunaweza kushirikiana tukalisafisha kanisa kwa pamoja.**

**27. PHILIP:** **Jamani lazima tuizingatie hali halisi.Sidhani utafanikiwa kuwashirikisha vijana wa Kiislamu katika shughuli ya kulisafisha kanisa.**

**28. LAYLA:** **Kwanini wasikubali ,Philip?Tuwaulize kwanza! Huo ndio mwanzo wa majadiliano…Au vipi?**

**29. HARRY:** **Hmm. Sikilizeni, mpango huu wa kusafisha kanisa ni wa muda mfupi tu lakini kwanini tusishirikiane kuanzisha kituo cha vijana,kitakachokuwa na klabu ya michezo kwa manufaa yetu sote?**

**30. DIRECTOR:** **Hmm… Kituo kitakachowaleta pamoja watu wa dini na tamaduni mbalimbali?Nimelipenda sana wazo hilo. Hata hivyo twendeni hatua kwa hatua! Kwanza tuanze kwa majadiliano.Maridhiano sharti yazishirikishe pande zote mbili husika.**

**31. LAYLA:** **Ningependa Mimi na Harry tuanze kwa kuzishawishi familia zetu zisitishe mivutano yao na ziliwachie Baraza la Maendeleo liisimamie ardhi hiyo itakayotumika kwa shughuli zitakazozinufaisha jamii zote.**

**32. PHILIP:** Nami p**ia nitazungumza na Babangu. Nadhani muda umewadia.Anaweza kuwaomba wahariri waandika uhariri unaoishauri jamii ifikie maridhiano..**

**33. MAT:** **Pia mimi naweza kuwatembelea vijana wa Madrassa, kuusikiliza mtazamo wao kuhusu ushirikiano wa muda mrefu.**

**34. HARRY:** ***(whispers)*** **Twende Layla, tunahitaji kuzugumza mambo fulani. Twende kule chini ya daraja la Mto Gori.**

**35. <u>BRIDGING MUSIC</u>**

**<u>Scene 3. Under Gori Bridge</u>**

**Harry, Layla**

**36. <u>SFX: River, birds, cars noise from a distance</u>**

**37. HARRY:** **Sawa hapa sawa kabisa…!. Hakuna Mtu anayeweza kutuona hapa chini ya Daraja. Sasa Layla nieleze, kwanini ulikasirika baada mjadala siku ile?**

**38. LAYLA:** **Ohhh. Um... Nadhani ni kwasababu ya wivu tu! Roshi alinifahamisha kwamba Marian alikuwa anakuandama sana! Na kwamba yeye ndiye aliyekupa mkufu ule…..**

**39. HARRY:** Ni kweli alikuwa akijaribu kunishawishi nijiunge na kanisa la Mchungaji Immanuel, lakini kusema kweli nilikuwa nimeyasahau kabisa mambo hayo ya mkufu.Philip aliuchukua baada ya kipindi Fulani.Nadhani ulidondoka tokea mfukoni mwake.

**40. LAYLA:** Hahh. Nadhani kuna jambo linalomsumbua Philip. Sasa tuyasahau hayo. Tuna mambo ya muhimu zaidi ya kuyafikiria.

**41. HARRY:** Ni kweli kabisa. Mimi na wewe sasa tunahitajika kwenda kuzungumza na Baba mdogo Askofu, na kisha baadaye Babako.

**42. LAYLA:** Baba hujiuliza kila wakati, … nini kilichomuingia Hassan mpaka akaamua kulishambulia kanisa kwa moto!Nadhani atalifurahia wazo la kurejesha amani kati ya familia zetu.

**43. HARRY:** Na baina yetu? Amani ?

**44. LAYLA:** Amani na Upendo Harry.

**45. <u>SFX: Kiss and sigh softly</u>**

**46. <u>BRIDGING MUSIC</u>**

**47. PHILIP/NARRATOR: Penzi lao lilikuwa limeanza kunawiri tena.Sikuwa na mwanya wowote!Ilinibidi nikubaliane na hali halisi.Wakati huo huo Kasisi Barnabus alikuwa ameanza kuuona umuhimu wa Ubuntu katika kanisa lake..**

**<u>Scene 4. In church</u>**

**Father Barnabus, Ishmail Omer, Hassan**

**48. <u>SFX: Organ music in the background. Echo on footsteps</u>**

**49. FATHER B:** *(angry)* **Bw Omer? Wewe Hassan? Unafanya nini hapa kanisani?**

**50. MR OMER:** *(softly to Hassan)* **Zungumza Mwanangu.**

**51. HASSAN:** *(shy)* **Kasisi Barnabus, samahani kwa yote niliyotenda. Kunradhi!.**

**52. FATHER B:** *(taken aback)* **Umm..unaomba radhi… sawa…ummm...**

**53. MR OMER:** **Kasisi, sisi sote tunamuabudu Mungu mmoja.Sisi tanamuita Allah, lakini ni Mungu mwenye huruma nyingi katika dini zote mbili.Mwanangu amekiri na ametubu. Na yuko tayari kufanya utakavyomuagiza.Mimi pia kama Babake nitawajibika…na ninauliza:Je tufanye kipi ili tuisawazishe hali hii?**

**54. FATHER B:** **Um...sawa..nadhani kwanza tusali. Tupige magoti na tuombe pamoja ..tushikane mikono na tumuombe Mungu atupe huruma zake ,kila mmoja kwa njia yake.**

**55. <u>SFX: Organ music up</u>**

**56. PHILIP/NARRATOR: Baadaye siku hiyo Chifu Dembele aliwasili nyumbani kwa kakake kama ilivyopangwa.Amesafiri kutoka sehemu za mashambani kuhudhuria kikao hiki.Pindi Harry na Layla walipoingia chumbani humo, wazee hao wawili walisimama kama ishara ya heshima.**

**Scene 5. At Father Barnabus'**

**Harry, Chief Dembele, Father B, Layla**

*57.* **ALL:** **(*Exchange polite greetings)***

**58. HARRY:** **Kasisi, baba mdogo, huyu ni Layla Omer**.

**59. CHIEF DEMBELE: Layla! Nimefurahi kukutana na wewe.**

**60. FATHER B: Wewe ni Dadake Hassan?**

**61. LAYLA: Ndio Kasisi.Na kwa niaba ya Familia yangu ningependa kuomba msamaha kwa yote yaliyotokea.**

**62. FATHER B: Layla – Mdogo wako Hassan na Babako walikuja kanisani mwangu leo alasiri!**

**63. LAYLA:** ***(surprised*) Walikuja …?**

**64. HARRY: (surprised)** …**Kanisani?**

**65. FATHER B:** Ndio.Pia walikuja kuniomba msamaha. Na kusema kweli niliuhisi unyenyekevu wao. Tuliomba pamoja na kuwaambia kwamba nitaitupilia mbali kesi hiyo iliyoko Polisi.

**66. CHIEF DEMBELE:** Ulifanya vizuri sana Kakangu. Naamini amani ni muhimu zaidi hapa Gori kuliko kipande kile cha Ardhi! ***(chuckles)***

**67. LAYLA:** Ahsante Kasisi Barnabus. Chifu Dembele ningependa kuchangia?

**68. CHIEF DEMBELE:** Endelea.. Tafadhali keti. Pia Harry ketini tuzungumze.

**69. SFX: moving wooden chairs, glasses, pouring water**

**70. LAYLA:** Mimi na Harry tuna mapendekezo.

**71. CHIEF DEMBELE:** Ehhe ,.. pendekezo gani hilo?

**72. HARRY:** Baba Mdogo, tungependa vijana kutoka jamii hii, wote waislamu kwa Wakristo…

**73. LAYLA:** Vijana wote-

**74. HARRY:** ...Kushirikiana kujenga kituo cha kijamii katika kipande kile cha ardhi.. ambacho kitaitwa…..

**75. HARRY+LAYLA:** …Kituo cha Mapatano!

**76. BRIDGING MUSIC UP**

**77. PHILIP/NARRATOR:** Nilijua kwamba siku hii ingeyabadili maisha yangu.Jinsi tulivyotangamana katika Chuo cha Ubuntu,tulivyojifunza kuyarithi majukumu yauongozi,kutafutasuluhu zamizozo kwa njia za amani.Jengine ni jinsi baba alivyobadilika na akawa tayari kuelezea mambo yaliyokuwa yakimsumbua.

**Scene 6. At the Layton-Browne's in the evening**

**Philip, Philip's father**

**78. SFX: Background TV /radio noise**

**79. PHILIP:** Baba – kuna nini?

**80. P's FATHER:** **Ai! Picha ile.!Heri ningekuwa nimeichoma miaka mingi tu iliyopita.**

**81. PHILIP:** **Yule mwanamke ni nani?Kwanini iko hapa juu ya meza yako ?**

**82. P'S FATHER:** **Philip. Ni hadithi ndefu …**

**83. PHILIP:** **Baba!Kipi kinachoendelea hapa? Niambie!**

**(Silence)**

**84. P's FATHER:** **Haaah! (Sobs into his hands)**

**85. SIG TUNE UP**

**86. OUTRO:**

**Naam hadi hapo tumefika mwisho wa kipindi cha Noa Bongo-Jenga Maisha Yako kwa leo!Harry na Layla walisameheana na kuufungua ukurasa mpya naye Hassan amemuomba Kasisi Barnabus msamaha.Ungana nasi tena kwa sehemu ya kumi na ya mwisho katika mfululizo wa mchezo huu 'Daraja la Gori,' uweze kufahamu kilichomtatiza Babake Philip kadhalika jinsi Familia za Harry na Layla zitakavyoichukulia mipango yao ya baadaye.Kumbuka ukiwa na maoni au ungependa**

**kukisilikiliza tena kipindi hiki pamoja na marafiki tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.!**

**END OF EPISODE 9**